Simulizi Ya:

# MTANDAO WA AJABU

Mtunzi: **Maumba SB**

E-MAIL: **saidmaumba01@gmail.com**

Simu: **0688923495**

…..Hii simulizi ni ya kufikirika na ya kubuni tu!, ikiwa imetungwa na mwandishi kijana kabisa…

**SAID B MAUMBA.**

Wala hairuhusiwi kunakili,kuchapisha upya au kusambaza kazi hii bila ya ruhusa kutoka kwa mwandishi na mtunzi wa kazi hii.Anayepatikana kwa e-mail ya: saidmaumba01@gmail.com

Tafadhali thamini juhudi za mwandishi ambaye ametumia muda wake mwingi sana kuandaa kazi hii.Tafadhali hii hadithi ni kwa matumizi yako tuu! Wewe kama wewe mara baada ya kujipatia kutoka kwa Mtunzi.Hakikisha kuwa….unajali nguvu na juhudi za mwandishi.

Kama mtu akihitaji…**please** mwambie aweze kujipatia ya kwake kutoka kwa mwandishi kwa kuweza kutuma e-mail kwenda saidmaumba01@gmail.com.

**SHUKRANI SANA !**

**MWANZO:….***storika sasa!!*

Ilikuwa ni majira ya saa sita za usiku. Nikiwa ndani ya chumba changu, nilikunja nne vizuri huku nikining'inia katika kiti kirefu cha ofisini chenye matairi sita chini. Macho kodo! Nikiwa nimekodolea kompyuta mpakato aina ya Dell Latitude D 630.

Kwenye skrini ya Laptop yangu, ilisomeka vyema profile picha yangu.

***D*a*n*i*e*l H*a*c*k*e*r**

**Miaka 19**

**Jiji: Dar es salaam.**

Japo niliketi kwenye kiti cha kuzunguka. Nilikosa usingizi na sikuwa na amani kabisa huku hamu kubwa ya kutaka kumfahamu yule aliyekuwa amenitumia message kwa njia ya e-mail hapo asubuhi ya saa 4 kasorobo, ikinikaa vizuri kwenye koo.

Ndiyo!, Leo asubuhi saa nne, nilipokea meseji yenye kuogopesha sana huku ikiandikwa kutoka kwa mtu asiyejulikana.

Basi niliendelea kuvuta subra kwenye kiti hicho.

Kwa mazingira ya nje yalikuwa shwari kabisa huku mvua ya rasharasha ikiendelea kunyesha. Upepo kiasi uliendelea kuvuma huku ukiufanya usiku huo kuwa tulivu mno. Hakukuwa na kelele zozote isipokuwa zile za mvua pindi ilipogonga kwenye paa la nyumba. Na kidogo mti uliokuwa dirishani kwangu pale ulipokuwa unavuma kutokana na kijiupepo mwendopole kilichokuwa kikiendelea.

Kwa mujibu wa meseji niliyoipokea saa 4 kasorobo asubuhi ilisomeka.

**>>>from Unknown<<<<<**

***“Usiulize mimi ni nani!.Ila wewe ni Daniel Hacker, miaka 19, unamiliki website ya MtumutuOnline?. Tunafahamu mengi sana kukuhusu wewe. Mipango yako na siri zako zote zipo hatarini”***

***“Usijaribu kufanya ujanja. Saa sita usiku hakikisha unakuwa online!”***

***"Ni lazima uwe online bila ya kukosa. Lasivyo!….."***

**>>>>kutoka kwa Asiyejulikana<<<<<**

Ilinibidi kuwa online hadi muda huo ambapo mbu wachache waliendelea kuniunga mkono kukesha hapo mbele ya laptop yangu. Wote tukisubiria ujio wa ujumbe kutoka kusikojulikana.

Nilipotaka kusinzia tu, Ghafla ujumbe mfupi ulitumwa ndani ya simu yangu bila ya kuonyesha namba ya mtu anayetuma.

**>>>>from uknown>>>>**

***"Your password please!?…."***

**>>>>from uknown>>>>**

***"Kwanza kwani wewe ni nani"***, niliuliza huku nikiingiwa na wasiwasi wenye mashaka makubwa mno.

**>>>from Unknown>>>>**

***"Nilishakwambia usiniulize mimi ni nani. Your password please…"***

**>>>>from uknown>>>>**

Meseji ilijibiwa hivyo kutoka kwa huyo huyo mtu asiyejulikana.

Akili yangu ilitetema sana baada ya kutetemeshwa na wingi wa wasiwaasi ulioniingia kwa muda huo. Nilijawa hofu kubwa mithili ya mapiramidi ya Misri.

Nilifikiria kuripoti kwenye kitengo kinachohusika na masuala ya uhalifu wa mitandaoni. Lakini nilikumbuka vyema ile meseji haswaa, pale aliposema kuhusu kutofanya ujanja ujanja wowote ule.

Pia nilifikiria mara mbili mbili vipi kama ni kweli watu hawa wanazo siri zangu?. Vipi kama ni kweli wanaifahamu mipango yangu mikubwa niliyoipanga hapo baadae?. Kama nikifanya ujanja yamkini likaniangukia jumba bovu.

Basi kichwani kwangu kulijaa alama nyingi za viulizo na mshangao huku mkono nikiwa nimeuseti usawa wa button ya **'Enter'**. Tayari kwa kutaka kutoa taarifa kwenye kitengo cha usalama wa mitandaoni.

Ndipo ilipoingia meseji nyingine kutoka kwa yule yule huku ikianza na utaratibu wake….. "From Unknown"

***"Usifikirie kubofya hicho kitufe. Utajihatarishia zaidi. Usalama wako ni kufuata tunachokuambia. Usichezee shilingi kwenye shimo la choo. Daniel, Your password please!….."***

Hii iliniogopesha zaidi. Macho yalizidi nitoka kodo! Mithili ya mjusi aliyebanwa na mlango. Pumzi nazo zilikuwa zikienda kwa kasi kama vile nilikuwa nakimbizwa na kikaragosi. Au, kibwengo mwenye kutisha sana.

*"Sasa wamejua juaje kama nilitaka kubofya kitufe hiki?.Ina maana huko waliko wanaweza kuniona?.Au ni nini hasa kinachoendelea kati yangu na kiumbe huyu nisiyemfahamu hadi saa hii?"*

Nilibaki nikijiuliza maswali ya aina hiyo kwenye viwanja mblimbali vya ubongo wangu. Bila ya kuweza kulijibu hata moja.

Nilijiuliza na kutafakari sana. Lakini hakuna jibu la maana lililonijia akilini mwangu.

Nilijiuliza je, niwape password yangu au nisiwape?. Vipi kama wakiipata na kunitosa mazima?.

Ndugu msomaji, nilikuwa katika hali ngumu mno.

Niligeuka na kutazama saa ya ukutani iliyokuwa juu kabisa usawa wa lilipokuwa kabati langu la nguo. Lakini niliona kama vile muda hauendi. Mishale ya saa ilienda taratibu kama mwendo wa bibi harusi. Nilitamani kukuche lakini ndio kwanza kiza kinene kilizidi kunenepeana na kuongezeka tu.

Mara nilijishika kichwani mara shavuni huku nikitafakari tu. Niwape, au nisiwape?. Vipi kama nikiwapatia My Password?. Nini kitanitokea?. Lakini siwajui ni akina nani hawa.

Kilichonichanganya zaidi ni vile wanavyodai kunifahamu zaidi. wamenifahamu vipi?. Kidume niliendelea kuumiza ndonga bila ya kupata ufumbuzi wowote ule.

Mara ghafla bin vuu ikaingia message kutoka kwa yuleyule…

**>>>>from uknown>>>>**

***"Usijichoshe kufikiria sana, kuhusu kutoa password yako. Labda ngoja tukuambie ulichokifanya tarehe 23/2… last Monday…shall we tell you?"***

Moyoni nilisita na kusema

"No!.. hadi hii secret issue mnaifahamu". Huku nikiwa nashangaa shangaa ndipo muda huohuo message ya pili nayo ikaingia kutoka kwake yuleyule…

***"Last Monday yani, tarehe 23/2. Uli-hack kwenye tovuti moja ya magemu ya kulipia, na kisha kucheza bure. Pia Uliweza kuingiza program ya siri (secret hidden program) ambayo kazi yake ni kufyonza taarifa na miamala ya pesa na kuweza kuiba kisha kuhamisha kwenye bank account yako.***

***Ulifanya kwa siri na utaalamu mkubwa sana ukidhani hakuna yeyote anayejua…, Hongera sana Daniel!."***

**>>>>from uknown>>>>**

Aisee!, ulikuwa ni mtandao wa ajabu sana.

Ujumbe huu kutoka kwenye mtandao wao ulizidi kunifanya niingiwe na hofu nyingi zaidi. Safari hii nilisikia utumbo kwa mbali uki-vibrate na kurukaruka ile mbaya yani.

Sasa nilianza kuamini kwamba hawa si watu wa kawaida. Na, huenda ni kweli kwamba wanazifahamu siri zangu nyingi sana. Na huenda ni watu wenye mtandao strong ulio powerful sana. Kwa sababu hakuna mtu ambaye angeweza kugundua kwa urahisi ule mtindo wa HACKING nilioufanya hapo Februari 23 kwenye tovuti moja kaali sana ya kulipia ya online games.

Hakuna ambaye angegundua hacking codes ambazo niliziingiza kwenye miamala na kuiba fedha za account za wacheza game katika mtandao huo. Naamini kabisa, hakuna ambaye angeweza kugundua…, ila huyu jamaa anayedai kutojulikana aliweza kubaini kila kitu. Tena alinianikia siri hiyo kama vile anasoma gazeti yani. Kwa kweli iliniogopesha sana!.

***"Usishangae Daniel. Simply type your Password"*** Alituma message nyingine ambayo ilizidi kuendelea kunitaka nitoe password yangu.

Walishanitisha na kunitetemesha vya kutosha sana. Yani hadi ujasiri wa kuanza kukataa ulishapungua polepole. Walishanidogodesha!.

Kinyonge kabisa nilichukua keyboard tayari kwa kuandika kitu na kutuma kwa jamaa. Taratiibu niliset vidole juu ya keyboard na kuanza kucharaza maandishi…

Japo yalikuwa ni maamuzi magumu lakini ndo hivyo tena nilishaandika.

Nilitafakari sana kisha nikafanya uamuzi wa kuwauliza tu. Ili niweze kufahamu mlolongo mzima wa wao kunishinikiza hivyo kwamba niwape Password kisha kujiunga nao.

***"Kwanini mnaitaka password yangu?"***, niliuliza. Tena sio kwa herufi ndogo bali ni kwa herufi kubwa ili kuonyesha msisitizo zaidi.

Haikuchukua hata sekunde tano ndipo king'ora cha meseji kililia twii! Twii…

**>>>>from uknown>>>>**

***"Hatuhitaji kuharibu siri yako hata moja Daniel. We have a BIG DEAL tunayotaka tuifanye pamoja na wewe Daniel. SO!..., tunahitaji password yako ili uweze kuwa ndani ya team yetu"***

**>>>>from uknown>>>>**

Mmh!. Niliguna kidogo baada ya kuusoma ujumbe huo ulioendelea kunivuruga zaidi. "Eti kufanya kazi pamoja na wao?", nilijiuliza mara mbilimbili kichwani. Swali hili liligonga na kujirudia rudia kichwani kama vile sauti ya mwangwi pangoni.

"Lakini mimi siwafahamu ninyi ni akina nani?.Sasa nitawaamini amini vipi?". Nilicharaza ujumbe na kuutuma hukooo! mahala kusipojulikana zilipotokea jumbe za yule Unknown Creature.

**>>>>from uknown>>>>**

***"Daniel!, Lakini sisi tunafahamu kwa kina kuhusu wewe. Je, hii haitoshi kwa wewe kutuamini. Au, mpaka tukufunulie ukurasa mwingine wenye siri zako ambazo unadhani hakuna anayezifahamu?. Fikiria Daniel"***

**>>>>from uknown>>>>**

Dah! Huyu jamaa aliendelea kunitia hofu moyoni. Alinifanya hata nisipate lepe la usingizi na badala yake niliendelea kujadiliana naye tu kupitia laptop yangu. Japokuwa hadi saa hiyo sikumfahamu.

Hata nilipotazama nje kupitia dirishani, kumbe mvua nayo ilishanyamaza kitambo sana. Lakini wala sikuweza kutambua pale ilipokata. Hii yote ni vile tu nilivyokuwa bize pale kutext na mtu asiyejulikana huku yeye akidai kunijua mimi kuanzia A mpaka Z.

Nikashika Keyboard. “Lakini wewe kunifahamu mimi haitoshi. Inabidi pia na mimi niweze kukufahamu. We trust much when we understand each other. Inabidi nikufahamu ili niweze kufanya hicho unachoniambia. I need to undersand WEWE NI NANI?. Kutokea wapi?”

Aisee sijui ulijitokeza wapi huu ujasiri wa kujibu hivi hususan kwenda kwa mtu nisiyemfahamu. Simfahamu lakini…, yeye ananifahamu.

**>>>>from uknown>>>>**

***“Daniel!, una haraka sana lakini kila kitu utaenda kukijua hivi karibuni kama kweli unataka kukijua. Hata mimi utanifahamu muda si mrefu…, ila yote hii haiwezekani bila ya wewe kufanya ninachokuambia.***